maamuzi sasa. Tubu na Umkiri Yesu Kristo sasa hivi yakuwa ni Bwana na mwokozi wa Maisha yako binafsi wa pekee.

*Waweza kumpokea kwa Imani kwa sala hii; Mungu Baba katika Jina la Yesu, asante kwa kunipenda na kumtoa mwanao wa pekee Bwana Yesu ili afe na kumwaga damu yake kwa ajili yangu ili niwe safi na kupatanishwa na wewe. Ninatubu dhambi zangu zote na kukubali Bwana Yesu uwe Mwokozi na Bwana wa maisha yangu. Unipe Roho wako Mtakatifu ili aniongoze katika kweli yote. Asante kwa kuniokoa leo. AMINA.*

Kwa msaada wa kiroho na maombezi, tafuta Kanisa la kiroho la Kikristo ujitambulishe na ukasali huko kwa uaminifu ili upate kukua kiroho.

*Waebrania 10:24-25, 2Timotheo 3:16-17, 1Petro 2:1-3, Ufunuo 3:5).*

Sisi tunapatikana
TAG MWENGE CHRISTIAN CENTRE
KARIBU NA HOSPITALI YA MAMA NGOMA.
KARIBU SANA.

**RATIBA YA IBADA ZETU.**

| | | |
|---|---|---|
| **Jumatano** | **Ijumaa** | **Jumapili Ibada ya Kwanza** |
| **Mafundisho** | **Ibada ya Maombi** | Saa: 12:30-3:00 Asubuhi |
| Saa: 10:30-12:00 | Saa: 10:30-12:00 | **Jumapili - Ibada ya Pili** |
| Jioni | Jioni | Saa:3:10 -7:00 Mchana |

**WASILIANA NASI!**
**MKURUGENZI IDARA YA UINJILISTI**
**NDG. SAMWEL ZAYUMBA SIMU:+255 713 250 034.**
**MWENGE DAR ES SALAAM, TANZANIA.**

ROMMEDIA GOSPEL TRACTS_4523_+255 713 310 721

# UTAMLAUMU NANI?



Ni jambo gani litakalokuepusha na moto wa milele ili kufika mbinguni? Utamlaumu nani utakapokufa na kuzikwa halafu unaingia motoni; ghafla unainua macho yako juu na kujikuta upo katika mateso makubwa?

**HUWEZI KUMLAUMU MUNGU;**

"Kwa kuwa Mungu hapendi mtu yeyote apotee, anapenda kila mmoja aokoke. "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanaye wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele
(Yoh 3:16)".

**HUWEZI KUSEMA;**

"Mimi sina dhambi" kwa kuwa Mungu anasema "kama kwa mtu, mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi (Rum 5: 12; 3:22-23)".

**HUWEZI KUSEMA;**

Nilijitaidi kuwa na dini nzuri, na moyo mzuri kwa hivyo Mungu hawezi kunitupa motoni. *Maana tunaokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo ambayo hiyo haikutokana na nafsi zetu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.* **(Waefeso 2 :8-9)".**

**HUWEZI KUSEMA;**

Sikuonywa kwa sababu Mungu hutumia njia mbalimbali kuonya watu mfano; mhubiri, machapisho ikawa pamoja na karatasi hii. Na huenda likawa ni onyo la mwisho la Mungu kwako (Waebrania 3:7-8).

**HUWEZI KUSEMA;**

Bado ninao wakati wa kutengeneza, kwakuwa hata kurudi kwake Yesu haijulikani siku wala saa, ni kama vile kifo kimjiapo mtu humjia bila maandalizi yeyote.
(Matayo 25 : 13 , 1 Wakorintho 15: 52).

**HUWEZI KUMLAUMU YULE;**

Aliyekupa karatasi hii, alikupa kwa ajili ya upendo alipotambua hatari inayokuja na anakuonya ili uelekeze mawazo na moyo wako kwa Mungu.

**HUWEZI KULAUMU MAZINGIRA;**

Kwa kuwa hakuna kizuizi cho chote kinachoweza kumzuia mwenye dhambi kufika kwa Mungu ikiwa anahitaji wokovu (Yeremia 5:40).

**HUWEZI KUSEMA;**

"Mimi nimetimiza sheria kwa kuwa Mungu anasema " Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote **(Yakobo 2:10)".**

**UNAWEZA KUSEMA HIVI ;**

Siamini kama kuna moto wa milele (Mt.13:42, Ufu. 21.8). Ndugu msomaji, unaweza kusema hauamini haya yote lakini kutokuamini kwako hakutobadili hali iliyoko na ukweli wake. Ni neno la kuaminika tena lastahili kukubalika kabisa ya kwamba Yesu Kristo alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi (1 Tim 1:15). Huna sababu ya kupingana na Mungu kwa kuwa mtu asiyeamini anamfanya Mungu kuwa ni muongo.

**HUNA LA KUJITETEA;**

Mwenye busara huyasoma mabaya na kujificha; bali wajinga huendelea mbele wakaumia (Mithali 22:3). Mwamini Bwana Yesu Kristo nawe utaokoka (Matendo 16:31).

NI JAMBO LA KIBINAFSI

Ewe Rafiki mpendwa, upendwaye na Mungu. Ni vizuri ufanye